

This booklet on Unexpected Pregnancy was developed by the Tanzania Home Economics Association with support from Our Bodies Ourselves. Other booklets and more information on the project are available at <http://www.ourbodiesourselves.org/tanzania>.

UJAUZITO USIOTARAJIWA

Una wasiwasi kwamba unaweza kuwa ujauzito? Wewe ni mmoja wa marafiki. Katika kipindi kimoja au kingine cha maisha yetu, takriban nusu ya wanawake wote hupata ujauzito bila kupanga. Kuna uwezekano mkubwa ukashindwa kuamini kama unaweza kuwa na ujauzito, iwe unahitaji mtoto au la.

Kama unafikiri una ujauzito, hatua ya kwanza ni kujaribu kutambua siku ya kwanza ya mara ya mwisho kupata hedhi. Hatua inayofuata ni kuchukua kipimo cha kuchunguza kama una ujauzito. Wakati unaweza kuwa na furaha na shauku juu ya uwezekano wa kuwa mama, vilevile unaweza kupata mshituko, aibu au kutokujiamini. Unaweza usiwe na uhakika kama uko tayari kuwa mzazi kwa sasa. Kuthibitisha ujauzito mapema hasa ndani ya mwezi wa mmoja kutakuwezesha kuwa na machaguo mengi zaidi ya kufanya.

NANI ANA MIMBA ZISIZOTARAJIWA?

- Zaidi ya mimba zisizotarajiwa milioni 3 hutokea kila mwaka nchini Marekani.
- Idadi ya wanawake wa Kimarekani milioni 3 ambao hawatumii njia za kuzuia kupata ujauzito wanawajibika kwa takriban nusu ya mimba hizi (asilimia 47) wakati wanawake wote milioni 39 wa Kimarekani wanaotumia njia za kuzuia kupata ujauzito hujumuisha asilimia 53 iliyobaki.

Ujauzito Usiotarajiwa (“Unexpected Pregnancy”). For more information, see: <http://www.ourbodiesourselves.org/tanzania>.

- Nyingi ya mimba zisizotarajiwa hutokea miongoni mwa wanawake wanaotumia njia za kuzuia mimba hutokana na kutotumia njia hizo ipasavyo.

Ikiwa unaogopa matokeo ya kipimo cha ujauzito, ni vizuri kumwona mtu mwenye utaalamu sahihi ili akupatie msaada unaohitaji. Kadiri utakapokuwa kwenye mchakato wa kutambua na kuchagua uamuzi sahihi, bado utakuwa na haki ya kupata msaada na ushauri wowote ule utakaohitaji, na haki ya kufanya maamuzi yako mwenyewe.

Ikiwa una ujauzito, unaweza kuwa unafahamu nini unataka kufanya mara moja, au unaweza kuona suala hilo ni lenye kukuweka katika wakati mgumu sana kimaamuzi. Weng wetu hubadilisha mawazo yetu pindi tunapokabiliana na ukweli kuwa tu wajawazito, hata kama tulifikiri kuwa tunafahamu kitu gani tungefanya. Jichukulie kwa uangalifu na jitunze vizuri. Kumbuka kuwa kuna msaada wa kukuongoza katika kipindi chote hicho, bila kujali mazingira uliyopo.

DALILI ZA UJAUZITO

Dalili za awali za ujauzito hutofautiana kutoka mwanamke mmoja hadi mwingine, na hata kutoka mimba moja hadi nyingine kwa mwanamke yuleyule. Zifuatazo ni dalili chache ambazo huwatokea wanawake wengi:

- Kukosa kabisa hedhi, kupata hedhi nyepesi au kipindi kifupi cha hedhi kuliko kawaida.
- Kulainika au kuongezeka ukubwa kwa matiti.
- Kiwango cha hisia cha chuchu kuongezeka.
- Kwenda haja ndogo mara kwa mara.
- Kujisikia uchovu usio wa kawaida

Ujauzito Usiotarajiwa (“Unexpected Pregnancy”). For more information, see: <http://www.ourbodiesourselves.org/tanzania>.

- Kichefuchefu na / au kutapika.
- Hamu ya chakula kuongezeka au kupungua.
- Kuwa na mihemko isivyo kawaida.

Kunaweza kuwa na sababu nyingine mbali ya ujauzito zinazoweza kusababisha upate baadhi ya dalili zilizotajwa hapo juu. Kama hutaki kuwa mjamzito, usichukulie tu kuwa tayari umeshapata mimba; tumia njia za kukinga mimba hadi pale utakapochukuwa kipimo cha kuthibitisha una ujauzito.

KUFAHAMU

Mwanamke yeyote aliyeanza kupata hedhi, ambaye hajakoma hedhi, na ambaye anajamiiiana na mwanaume kwa kuingiliwa ukeni anaweza kupata mimba bila kutarajia. Hata kama una umri wa miaka kumi na nne, au arobaini na tano, njia ya kuzuia mimba unazotumia zinaweza kushindwa kufanya kazi inavyotakiwa, hata iwe ni kufunga mirija ya uzazi ya mwanamke. Inawezekana, ingawa kwa nadra sana, ukapata ujauzito bila kuingiliwa endapo mbegu za kiume zitakaribia sehemu yako ya kuingilia ukeni. Kama unahisi kuwa una mimba kwa sasa, jaribu kuchukua kipimo cha mimba ndani ya saa 24.

Takriban nusu ya mimba kwa wanawake wenye umri zaidi ya miaka arobaini hutokea kwa bahati mbaya, kiwango cha juu zaidi kuliko makundi mengine ya kiumri isipokuwa wanawake wenye umri mdogo/matineja; kwa mimba hizi, wanawake wenye umri zaidi ya miaka arobaini hutoa mimba kwa kiwango kikubwa zaidi kuliko makundi mengine ya kiumri katika jamii.

Ni chini ya saa 72 tangu tendo la kujamiiiana au kubakwa lilipofanyika ndipo unaweza kuzuia mimba kwa kutumia njia za dharura za kuzuia mimba. Wasiliana na mtoa huduma wako wa afya au Simu ya moja kwa moja ya huduma ya Dharura ya Kuzuia Kupata Ujauzito: 1-800-584-9911.

Ujauzito Usiotarajiwa (“Unexpected Pregnancy”). For more information, see: <http://www.ourbodiesourselves.org/tanzania>.

Katika umri wa miaka 45, nilidhani kuwa naufahamu mwili wangu vizuri; unaweza ukadhani kila kitu kiko chini ya udhibiti wako. Nilikuwa nimechoka sana, na hedhi yangu ilikuwa nyepesi, lakini sikudhania kabisa kama ninaweza kuwa nimepata ujauzito. Rafiki yangu aliniuliza “ Inawezekana ukawa mjamzito?” Nilinunua kipimo na kujipima wakati wa chakula cha mchana. Nilikuwa na mchachariko sana na nikakigeuza kipimo juu chini, na kilionyesha sikuwa na ujauzito. Nilijipima tena siku iliyofuata. Kilionyesha kuwa nina ujauzito.

KIPIMO

Njia rahisi ya kufahamu ni kufanya kipimo cha mimba cha nyumbani, ambacho hupima mkojo wako wa kwanza wa asubuhi. Kipimo hiki ni rahisi kutumia. Kinapatikana katika kitengo cha uzazi wa majira cha maduka ya dawa, na kitakugharimu kati ya dola 6 na 12. Fuata maelekezo vizuri. Kipimo kina uwezo wa kutambua ujauzito kuanzia muda uliokosa hedhi, kama wiki mbili hivi baada ya kuanguliwa yai.

Kliniki za uzazi wa majira, vituo vya huduma za afya vya wanawake, na ofisi za ofisi za kitabibu zinafanya vipimo vya mkojo na damu. Kipimo cha damu kina uwezo wa kugundua ujauzito kuanzia siku ya sita hadi ya nane baada ya yai kuanguliwa. Vipimoinavyojulikana kama Monoclonal Antibody Tests, hugundua human chorionic gonadotropin (hCG), homoni inayopatikana kwanza kwenye kwenye mkondo wa damu na halafu kwenye mkojo wakati wa ujauzito. Kuwa mwangalifu usifikirie kwamba endapo matokeo ya kipimo yataonyesha huna ujauzito basi inamaana hivyo. Matokeo ya kipimo yanaweza kuonyesha huna ujauzito kwa sababu kipimo hakikutumika kwa usahihi au kwa sababu ulipima ujauzito mapema sana wakati kiwango cha hCG kikiwa chini sana kuweza kugundulika.

Ujauzito Usiotarajiwa (“Unexpected Pregnancy”). For more information, see:
<http://www.ourbodiesourselves.org/tanzania>.

Kuwa makini sana na baadhi ya kliniki, mara nyingine zinajulikana kama vituo vya msukosuko wa mimba au mbadala wa kutoa mimba, zinazotoa huduma ya kupima ujuzito na ushauri bure ili kukufanya uondoe kabisa wazo la kutoa mimba, au kukufanya ukubali kuasilisha mtoto na kampuni yao ya uwakala wa kuasili watoto. Unapokuwa unatafuta kupima ujuzito, matibabu, au ushauri nasaha, ni kitu cha kawaida kujisikia nafuu unapokutana na kliniki kama hizi, na vilevile kuwa dhaifu mbele yao. Wataalamu wa afya pia, kwa kupenda au bila kujijua, wanaweza pia kukuchukulia kwa mtazamo tofauti kulingana na umri, mbari, ulemavu ulio nao au sababu yoyote ile nyingine. Bila kujali uko katika mazingira gani, unapaswa kupata msaada unaokidhi mahitaji yako na usiokuchukulia kwa mtazamo wowote ule.

PUMZI YA AHUENI

Ikiwa ulihisi kuwa una ujuzito lakini ikaja kuonekana kuwa si hivyo – na hautaki kweli kuwa mjamzito – zifuatazo ni baadhi ya dondoo za kuzuia mimba sisizotarajiwa:-

- Chagua njia ya kuzuia mimba inayokufaa; kila siku kuna maboresho na machaguo mapya ya njia za kuzuia mimba (Tazama Sura ya 18, “Kupanga Uzazi.”)
- Endapo utakuwa umebakwa, tafuta msaada. Piga Simu ya moja kwa moja ya Msaada ya Kitaifa ya Ukatili wa Majumbani: 1-800-799-7233, au Mtandao wa Klitaifa wa Ukatili, Ubakaji na Ngoni kwa Maharimu: 1-800-656-HOPE (4673), na rejea Sura ya 8 “Unyanyasaji na Ukatili.”
- Fahamu wapi pa kupata kinga ya dharura ya mimba. Unaweza kuhitaji kutembea na kifurushi cha kinga hii kwa mahitaji ya dharura.
- Zungumza na mshauri nasaha katika kliniki ya afya ya wanawake au ya uzazi wa majira.

Ujuzito Usiotarajiwa (“Unexpected Pregnancy”). For more information, see: <http://www.ourbodiesourselves.org/tanzania>.

PUMZI YA KUJUTIA

Ikiwa si mjamzito lakini ukatambua kuwa unatamani ungekuwa mjamzito, sasa utakuwa na muda wa kujiandaa. Kufahamu zaid kuhusu huduma kabla ya kupata ujauzito na kubeba mimba, tazama Sura ya 17, “Kufikiria kuwa Mzazi.”

IMETHIBITISHWA: UNA UJAUZITO

Kama utagundua kwamba una ujauzito, utahitaji muda kukubali na kukabiliana na tarifa hii na hisia za kila aina ambazo zitafuata. Hata kama utafurahia kuwa mjamzito, wewe na mwenzi wako mnaweza kujiona kiroho, kihisia na kiuchumi hamko tayari kuwa wazazi kwa sasa. Jiamini; unaweza kugundua lipi ni jema kwako. Kufikiria kwa uangalifu, kuongea na marafiki wa karibu au wanafamilia, ushauri pamoja na maandiko yanaweza kukusaidia kufikiria mambo ambayo yako ndani ya uwezo wako.

KUCHUKUA MUDA MREFU KUGUNDUA

Si kitu cha ajabu kuwa na ujauzito wa zaidi ya miez miwili bila kujitambua. Utamaduni na malezi ya kifamilia zetu vinaweza kutusaidia kuelewa mabadiliko katika miili yetu. Wengi wetu hufikiri tuna matatizo katika mfumo wa chakula, hofu au mafua. Baadhi yetu, tumeshajiweka katika hatari mbalimbali bila ya kupata ujauzito au tumejaribu kwa muda mrefu kupata ujauzito bila kufanikiwa, kiasi kwamba kwamba tunafikiri tu wagumba. Kwa baadhi yetu, haituingii akilini, na hatukubaliani kabisa na dalili hizi. Kwa wengine, hatutaki kufanya maamuzi kuhusu ujauzito, hivyo tunasubiri hadi tunafike mbali kiasi kwamba tunakuwa tumebakiwa na machagu machache sana. Kwa sababu zozote zile zinazoweza kukuchelewesaha, ni suala la muhimu kupata huduma za afya mapema iwezekanavyo kwa faida yako ya baadae na kwa afya ya mtoto anayetarajiwa.”

Ujauzito Usiotarajiwa (“Unexpected Pregnancy”). For more information, see:
<http://www.ourbodiesourselves.org/tanzania>.

Nilifikiri nina ujauzito kwa sababu nilikosa hedhi, lakini nilijaribu kutoifikiria. Mama yangu asingeniruhusu kulisahau jambo hili, hivyo sikutaka kumweleza. Sikutaka kuwaeleza rafiki zangu kwa sababu nilihofia neno hili lingevuma shule nzima. Hatimaye nilimweleza mpenzi wangu, naye aliamua ni wapi nikapate vipimo, lakini nilihofu. Ningeweka miadi kwenda kliniki na kisha nisingeenda. Wiki zilipita, na hatimaye niliongea na mshauri nasaha. Alikuwa mzuri sana. Alinieleza kila kitu, na nikapata vipimo, lakini tayari nilikuwa na ujauzito wa miezi mitano.

KUAMUA CHA KUFANYA

Mara baada ya kugundua kuwa una ujauzito, hatua inayofuata ni kuamua ama kubaki nayo au kuitoa. Kama utaamua kuitunza mimba, unaweza kuamua kumlea mtoto peke yako, au alelewe kwa kuasiliwa au chini ya huduma ya kufikia.

Wengi wetu huwa tunajihisi kutatizwa kihisia kwa muda mrefu kabla ya kuchagua hatua inayofuata. Mwili wako utakuwa unapitia kipindi cha mabadiliko ya kihomoni yatakayoathiri hisia zako. Chukua muda kusikiliza silika na mahitaji yako. Ni tendo la kimaadili na la litakaloonyesha kuwajibika kwako kufanya uchaguzi sahihi kwako. Kama utaacha ujauzito uendelee bila kupata huduma ya afya, utajipunguzia machaguo yako, na unaweza kukiumiza kijusi kilichopo tumboni. Zaidi ya hapo, wasichana wenye umri kati ya miaka 13 na 19 – ambao miili yao bado inakomaa na ambao mara nyingi wana tabia ya kuepuka kupata huduma ya afya – wako katika uwezekano wa kupoteza maisha kutokana na vyanzo vinvyohusiana na ujauzito mara nne zaidi ikilinganishwa na wanawake watu wazima. (Kwa maelezo zaidi na maswali kukusaidia kupata mwongozo wa mawazo na utafiti wako, tazama Sura ya 17, “Kufikiria kuwa Mzazi.”)

Makampuni ya bima yanachukulia ujauzito kama hali ambayo ipo tayari. Hii inamaanisha kwamba kama bado hauna bima, hawatakupatia huduma

hiyo. Na kama unayo bima, huduma hii haitahusika na ujauzito wala matatizo yanayoweza kujitokeza kutokana na ujauzito. Kujifungua kunagharimu kama dola 6000 na matatizo kutokana na kujifungua kama dola 2000 hivi kwa siku. Kama hauna, au una kipato kidogo, unaweza kupata huduma ya bima kutoka serikalini (Medicaid) ambayo inagharamikia ujauzito wote. Na panapokuwa na dharura, hospitali hawawezi kukukataa. Kwa maelezo zaidi, tazama, “Huduma kwa Wanawake Wajawazito Bila Bima ya Afya” kwenye ukurasa wa 427.

UKWELI KUHUSU BAADHI YA FIKRA POTOFU ZILIZOZOELEKA

- Mtoto hataboresha moja kwa moja uhusiano wako na mpenzi wako.
- Maumivu ya kutoa mimba sio makali zaidi kuliko uchungu wa kujifungua.
- Kutoa mimba sio ghali sana ukilinganisha na kupata mtoto.
- Kutumia dawa za kulevya mwanzoni mwa ujauzito kunakidhuru kujusi kilicho tumboni.
- Kuasiliwa mtoto wako hakukutengi nae moja kwa moja.
- Wanaume wanaweza kumpenda na kumlea mtoto kama wanawake wanavyoweza kufanya.

NANI WA KUMTEGEMEA

Mpenzi mwenye mapenzi na anyejua kulea anaweza kukupatia msaada mzuri sana kadiri utakapokuwa unakabiliana na ujauzito usiutarajia. Lakini hata kama hautakuwa na mtu kama huyo maishani mwako, unastahili na unahitaji kuheshimiwa wakati wote wa ujauzito na katika kufanya maamuzi.

SHINIKIZO LA KIFAMILIA

Ujauzito Usiotarajiwa (“Unexpected Pregnancy”). For more information, see: <http://www.ourbodiesourselves.org/tanzania>.

Wengi wetu tuna ndugu mmoja anayeamini kuwa yeye ndiye anaelewa lipi ni jema kwa kila mtu kwenye familia. Baadhi yetu pia tuna mama au ndugu wengine ambao siku zote humkaribisha mtoto anayezaliwa nyumbani mwao na hututaka tuitunze mimba na kumlea mtoto. Hii inaweza ikawa ni kwa sababu ya imani zao za kidini, majonzi waliyonayo baada ya kuwa wamempoteza mtoto mwingine, au utambulisho wao kama walezi wazuri wa watoto. Wengine kati yetu tuna wazazi ambao wanaoona tunawaaibisha na wanahofia athari ambazo mtoto atawaletea.

MWENZI MWENYE UTAYARI

Mwenzi wako anaweza kuwa na sababu za kukutaka kuitunza mimba au kuitoa, lakini hata sababu zake “nzuri” zinaweza zisijali lililo jema kwako au kwa mtoto. Na wakati mwingine, sababu zake zinaweza zisiwe “nzuri” sana, kwa mfano, anaweza kufikiri kwamba mtoto anaweza kuubadili uhusiano wenu unaoyumbayumba kuwa uhusiano imara na wa kuvutia. Au anaweza kumtumia mtoto kama sababu nyingine ya kutawala maisha yako.

Kama hali hizi zitajitokeza, amini silika zako na tafuta msaada. Kama wale wakupendao wana mitazamo isiyobadilika juu ya kitu unachotakiwa kufanya, unaweza kuhitaji msaada kusimama kinyume na mawazo yao, ama kusubiri hadi utakapokuwa umefanya uamuzi kabla ya kuwataarifu. Wakati mwingine kufanya kile moyo wako unataka kunamaanisha kupingana na matakwa yao.

Umaskini ni uhalisia wa kila siku kwa akina mama wengi walio na umri mdogo pamoja na watoto wao. Ndani ya miaka mitano baada ya kuzaliwa kwa mtoto wa kwanza, karibu nusu ya wazazi walio na umri mdogo na zaidi ya robo tatu ya akina mama walio na umri mdogo ambao hawajaolewa hutumia huduma za bure za ustawi wa jamii. Wanawake wenye umri mdogo wanaokabiliana na ukatili wa majumbani (takriban

theluthi moja ya wanawake wote wenye umri mdogo walio katika mahusiano) hupigwa zaidi baada ya kuolewa.

Kutafuta mshauri nasaha, piga simu kwa daktari wako, kampuni inayokupatia huduma ya bima, kituo jirani cha afya, au kliniki ya uzazi wa majir ailiyo karibu nawe. Yeyote utakayeamua kuzungumza naye anatakiwa awe msikivu na tayari kukusaidia na asiwe mwenye kutoa hukumu. Ili kumpata mtoa huduma wa afya au mshauri nasaha, piga simu kwa Shirikisho la Kitaifa la Kutoa Mimba kwa kutumia namba yao ya moja kwa moja iliyo wazi saa 24 kwa siku: 1-800-772-9100.

UTOAJI MIMBA

Utoaji mimba ni salama na unaruhusiwa kisheria nchini Maekani, ingawa hali yako kiuchumi, umri wako (ikiwa uko chini ya miaka kumi na sita), na mahali unapoishi kunaweza kukifanya kitendo hiki kikusababishie tabu. Muda salama na rahisi zaidi, na utakaoweza kumudu ni ndani ya kipindi cha miezi mitatu ya ujauzito (inahesabiwa kuanzia wakati wa hedhi yako ya mwisho). Ni vigumu sana kutoa mimba baada ya wik kimi na mbili kupita (kwa maelezo zaidi, tazama Sura ya 20, “Utoaji Mimba”).

KUTUNZA MIMBA

Kama utaaamua kuitunza mimba yako kwa kipindi chote cha miezi tisa, ni muhimu kupata huduma ya matibabu sasa. Acha kutumia pombe, dawa za kulevya, vidonge vya lishe, dawa za mitishamba, dawa za kupanga uzazi, na dawa za kujinunulia mwenyewe mpaka umepata ushauri au maelekezo kutoka kwa mtoa huduma wa afya. Kama unatumia dawa za kuandikiwa na daktari, mpigie simu mtoa huduma wako wa afya mara moja (kwa maelezo zaidi, tazama Sura ya 21, “Ujauzito”).

Ujauzito Usiotarajiwa (“Unexpected Pregnancy”). For more information, see: <http://www.ourbodiesourselves.org/tanzania>.

KULEA WATOTO

Watoto huwa wepesi sana kujirekebisha na wenye kuzoea mazingira pale wanapokuwa na mlezi thabiti na mwenye kujua kulea kihisia na wanapokuwa hawabugudhiwi, wanalishwa vizuri na kupatiwa usalama wa kutosha. Kadiri watoto wengi zaidi wanavyokua bila uwepo wa mtu wanayeweza kumwita baba, huku wazazi wa kike wakiwezesha zaidi kiuchumi na kujitegemea, inakubalika kijamii kwa sisi kulea mtoto peke yetu. Tunaweza pia kuamua kulea pamoja na baba wa mtoto wetu.

Nilikuwa kwenye uhusiano imara, wa muda mrefu na jamaa aliyekuwa akinisaidia sana ambaye nilijua angekuwa nyuma yangu katika kila jambo nitakaloamua kufanya. Nilitumia wiki nzima nikifikiria, nikishangaa, nikiumia moyoni, na kuandika. Mwishoni, niligundua kuwa nilihitaji kuwa mzazi. Nilimweleza mwenzi wangu kwamba angeweza kuondoka kwa sasa, au angeweza kubaki na kuwa baba wa mwanangu. Ninafurahi kuwa alikuamua kubaki. Nimemweleza binti yangu hadithi hii mara kwa mara. Binti yangu ana miaka mitatu kwa sasa. Ni moja kati ya hadithi anazozipenda zaidi. Nataka kuhakikisha anafahamu kuwa sikulazimishwa katika “kumpata” na nilichagua kuwa mama yake.

KULELEWA MTOTO

Katika kipindi chote cha historia, kuchangia kulea mtoto katika familia kubwa na miongoni mwa marafiki kumesaidia kuhakikisha kwamba watoto wengi Kadiri inavyowezekana wanapata fursa ya kukua. Utaratibu huu ni wa kawaida kabisa nchini Marekani na duniani kote kwa ujumla. Dhumuni ni kukupatia muda wa kutatua matatizo yako. Tafuta mwanasheria wa kukukusaidia katika kupata ulezi wa mtoto usio rasmi au mfumo wa malezi wa serikali ulio rasmi. Ni muhimu

Ujauzito Usiotarajiwa (“Unexpected Pregnancy”). For more information, see: <http://www.ourbodiesourselves.org/tanzania>.

kuhakikisha kuwa mlezi wa mtoto wako ataweza kufanya maamuzi kuhusu masuala ya kielimu na matibabu utakapokuwa haupo. Huna budi pia kujifunza hatua zipi za kufuata ili kupata tena nafas ya kumlea mwanao. Hasa katika mfumo wa malezi rasmi, unajiweka katika hatari ya kupoteza haki zako za kuwa mzazi moja kwa moja. (Kwa maelezo zaidi, tazama “Kulelewa Mtoto” [W46] kwenye tovuti, www.ourbodiesourselves.org.)

KUASILI MTOTO

Nilianza kwa kutazama maisha yangu kwa undani, na ni aina gani ya mzazi ninaweza kuwa, na ni aina gani ya maisha ya mtoto wangu nilitaka yawe. Ilinichoma kama mkuki ndani ya moyo wangu: sikuwa tayari, wala hata sikukaribia kuwa tayari kuwa mama. Sikuwa na kipato cha kutosha kuniwezesha kumtunza mtoto. Ni kweli, kulikuwa na msaada wa serikali...lakini sikuwa tayari kuona mwanangu akilelewa kwa msaadawa ustawi wa jamii. Ninawafahamu watu ambao wamefanya hivi, na sio rahisi. Sikutaka fedheha kama hiyo kwa mwanangu. Nilitaka binti yangu aishi kwenye nyumba imara, na sikuwa hata na uwezo wa kulipia kodi. Hakukuwa na baba karibu katika kipindi hicho. Sikutaka aina hiyo ya maisha kwa mwanangu. Hivyo niliwaza sana, nililia sana, nakapitia upya mawazo na hisia zangu, na hatimaye niliamua kwamba uamuzi bora utakuwa kumtoa mtoto wangu kwa ajili ya kuasiliwa.

Mpaka kwenye miaka ya 70, ilikuwa kitu cha kawaida kwa familia za kizungu za tabaka la kati kuwaficha watoto waliozaliwa katika mahusiano “yasiokubalika”. Mara nyingine wanawake wasioolewa ambao walipata ujauzito walipelekwa mahali pengine mbali na nyumbani na kulazimishwa kuwatoa watoto wao kwa ajili ya kuasiliwa. Kwa sasa, utaratibu wa kuasili mtoto kwa usiri unachukuliwa kama kitendo chenye madhara kisaikolojia kwako na kwa mtoto wako. Siku hizi kina mama wengi wanachagua kufuata taratibu za wazi za kuasili, hivyo kupata pia fursa ya kuendelea kuwa na mawasiliano na watoto wao. Endapo utachagua

Ujauzito Usiotarajiwa (“Unexpected Pregnancy”). For more information, see: <http://www.ourbodiesourselves.org/tanzania>.

kumtoa mtoto wako kwa ajili ya kuasiliwa kwa kufuata utaratibu usio wazi, hakikisha unachagua kampuni ya uwakala wa kuasili ambayo itatunza taarifa zako kwa ajili ya kumpatia mtoto wako na familia iliyomuasili ikiwa wataziomba. Pia hakikisha kuwa kampuni hiyo itakusaidia kufahamu namna mambo yanavyoendelea baadaye, hata kama kwa sasa unafikiri hautotaka kusikia tena kutoka kwao.

Kuasili mtoto unaweza kuwa uamuzi mgumu kufanya. Ikiwa utaamua kufuata njia hii, unaweza kuhudumiwa vizuri kwa kutengeneza mpango wa makusudi wa kuasili pamoja na mshauri wa mambo ya kuasili na kupitia kampuni yenye sifa za kutosha. Kampuni nzuri itagharamikia huduma zako za kisheria na ushauri na haikupatii pesa. Inakuhudumia wewe kama mteja, na siyo familia inayoasili mtoto. Ili kuepuka kuhudumiwa na kampuni isiyostahiki, piga simu Kituo cha Taifa cha Kunachokusanya na Kusambaza Taarifa kuhusu Kuasili kwa namba: 1-888-251-0075, na ulizia namna ya kuwasiliana na mtaalamu wa kuasili aliyeko jimboni mwako. Majimbo mengine yanazitaka familia kufanyiwa tathmini kwanza. Ikiwa hakuna utaratibu kama huu kwenye jimbo lako, jaribu kuwa na vigezo vyako mwenyewe vya familia inayofaa.

Ni utaratibu wa kawaida kwako wewe kama mama mzazi kuchagua familia ya itakayomuasili mtoto wako kutoka kwenye orodha ya waombaji wengi ili kuhakikisha mtoto wako atalelewa kwenye mazingira mazuri kadiri inavyowezekana. Kama hukupewa fursa hii, unaweza kutafuta kampuni nyingine. Makampuni mengi yanazitaka familia zinazoasili kutoa taarifa ya kila mwaka ya maendeleo ya makuzi ya mtoto kwa mama yake mzazi. Inawezekana kumuandikia mtoto barua na zikahifadhiwa kwenye faili kwa ajili ya kumbukumbu ya baadaye ya mtoto.

Kumekuwa na mabadiliko mengi kwa kipindi cha miaka 20 iliyopita katika kuasili watoto kutoka mbari tofauti. Endapo unadhani watakuathiri, hakikisha kampuni ya uwakala wa kuasili watoto inayokuhudumia inakwenda na wakati kuhusu masuala hayo. Kampuni nzuri itaweka kipaumbele katika kuhakikisha

historia ya mtoto na ile ya familia inayotaka kumuasili hazitofautiani sana. Kama itashindikana, jaribu kutafuta familia yenye mahusiano na jamii yenye maadili yanayolingana na yako. Ikiwa mmoja wenu kati yako au baba wa mtoto wako ni Mmarekani wa Asili, Sheria ya Wahindi Wekundu ya Matunzo ya Bure ya Ustawi wa Jamii kwa Mtoto ya mwaka 1978 inaweza kuathiri utaratibu mzima wa kuasili. (Kwa maelezo zaidi, tazama tovuti ya Chama cha Taifa cha Wahindi Wekundu cha Matunzo ya Bure ya Ustawi wa Jamii kwa Mtoto, www.nicwa.org.)

Unaweza pia kupata familia ya kumuasili mwanao kupitia tangazo la magazeti, msaidizi wa kuasili watoto wa kujitegemea, mtaalamu wa afya, au mwanasheria. Katika mazingira kama haya, huna budi kutengeneza mpango mzima wa kuasili moja kwa moja na wazazi na/au mwanasheria wao. Lakini kaa ukifahamu kuwa mwanasheria wao ataweka maslahi ya wateja wake kwanza mbele, sio yako. Iwe umeamua kuchagua utaratibu binafsi wa kuasili ama kwa kupitia kampuni ya uwakala, inashauriwa kuwa na mwanasheria na mshauri wako binafsi. Mshauri wa kuasili anaweza kufanya kazi na baba mzazi wa mtoto na familia zenu zote mbili pia.

KWA KUWA UMESHAFANYA UAMUZI WAKO

Ni muhimu ukawa mtaratibu. Njia yoyote utakayoamua kuafuata, unaweza ukahuzunikia njia ambayo hukuichukua. Huzuni ni kitu cha kawaida. Haimaanishi kuwa umefanya uamuzi mbaya, ila kwamba unasikitika kwa kupoteza jambo fulani. Kumbuka kuwa unahitaji msaada katika kipindi hiki. Kadiri unavyofahamu machaguo na hisia zako vizuri zaidi, ndivyo utakavyopata nguvu ya kuishi maisha yanayoridhisha.

Ujauzito Usiotarajiwa (“Unexpected Pregnancy”). For more information, see:
<http://www.ourbodiesourselves.org/tanzania>.